TANGAZO LA SERIKALI Na. 619 la tarehe 19/7/2024

SHERIA YA SHULE YA SHERIA TANZANIA,
(SURA YA 425)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 20(1)(d))*

KANUNI ZA USTAWI, MWENENDO NA NIDHAMU YA WANAFUNZI ZA MWAKA 2024

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Tasfiri.

SEHEMU YA PILI
MWENENDO WA WANAFUNZI

3. Serikali ya wanafunzi.
4. Akaunti ya Jumuiya ya Wanafunzi.
5. Mawasiliano.
6. Mikusanyiko nje ya Shule.
7. Ruhusa.
8. Kukusanya fedha.

SEHEMU YA TATU
MASUALA YA NIDHAMU

9. Kulinda taswira ya Shule.
10. Mamlaka ya nidhamu.
11. Mshauri wa Wanafunzi.
12. Kamati ya Ustawi na Nidhamu ya Wanafunzi.
13. Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wanafunzi.
14. Malalamiko.
15. Rufaa.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA JUMLA

16. Mali za wanafunzi.
17. Malazi na chakula.
18. Mahitaji maalumu.
19. Mavazi.
20. Huduma za maktaba.
21. Gharama za kusimamishwa masomo.
22. Mazishi.
23. Makosa ya jinai.

MAJEDWALI

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

SHERIA YA SHULE YA SHERIA TANZANIA,
(SURA YA 425)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 20(1)(d))*

KANUNI ZA USTAWI, MWENENDO NA NIDHAMU YA WANAFUNZI ZA MWAKA 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1.** Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Ustawi, Mwenendo na Nidhamu ya Wanafunzi za Mwaka 2024.

Tafsiri

**2.** Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Usimamizi iliyoanzishwa na kifungu cha 15 cha Sheria;

"Kamati" maana yake ni Kamati ya Ustawi na Nidhamu ya Wanafunzi iliyoanzishwa chini ya kanuni ya 12;

"Mkuu wa Shule" maana yake ni Mkuu wa Shule aliyeteuliwa chini ya Kifungu cha 13 cha Sheria;

"Mshauri wa Wanafunzi" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na Bodi kuwa na jukumu la kushughulikia ustawi wa wanafunzi;

"mtahiniwa" maana yake ni mtu aliyesajiliwa kwa ajili ya kufanya mtihani;

"mwakilishi wa wanafunzi" maana yake ni mwakilishi wa wanafunzi aliyechaguliwa na wanafunzi kuwakilisha maslahi ya wanafunzi kwenye mamlaka ya Shule;

"mwanafunzi" maana yake ni mtu aliyesajiliwa na Shule kufanya mafunzo kwa muda maalumu ulioainishwa na mtaala husika;

Sura ya 425

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania; na

"Shule" maana yake ni Shule ya Sheria Tanzania iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria.

SEHEMU YA PILI
MWENENDO WA WANAFUNZI

Serikali ya wanafunzi

**3**.-(1) Kutakuwa na serikali ya wanafunzi itakayojulikana kama Jumuiya ya Wanafunzi wa Shule ya Sheria itakayokuwa na jukumu la kusimamia masuala ya wanafunzi yanayohusiana na taaluma, jamii na burudani.

(2) Jumuiya hiyo itakuwa ni chombo pekee kinachowawakilisha wanafunzi ndani ya Shule.

(3) Malengo ya Jumuiya yatakuwa kama yalivyoainishwa katika Katiba yake.

Akaunti ya Jumuiya ya Wanafunzi

**4.**-(1) Jumuiya ya Wanafunzi itakuwa na akaunti yake ya Benki kwa madhumuni ya kuweka fedha kwa ajili ya kusimamia shughuli zake.

(2) Uongozi wa Jumuiya ya Wanafunzi unaomaliza muda wake utaacha kiasi cha fedha kisichopungua asilimia tano ya makusanyo yote ya mwaka yanayotokana na michango ya wanafunzi.

(3) Uongozi wa Jumuiya utakaoshindwa kutekeleza masharti yaliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (2) utalipa fedha hizo.

(4) Akaunti ya Jumuiya ya Wanafunzi itakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu wa Shule katika kila mwaka wa mafunzo.

Mawasiliano

**5**.-(1) Mawasiliano yote yatakayofanywa na Jumuiya ya Wanafunzi kwenda nje ya Shule yatatakiwa kupata idhini ya Mshauri wa Wanafunzi.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mshauri wa Wanafunzi anaweza kukataa kutoa idhini ikiwa suala linaloombwa ni kinyume na taratibu na kanuni za Shule.

Mikusanyiko nje ya Shule

**6**.-(1) Mwanafunzi mwenye nia ya kushiriki katika mkutano, mkusanyiko, mdahalo au majadiliano

yanayohusiana na masuala ya Shule atatakiwa kupata idhini ya maandishi ya Mshauri wa Wanafunzi.

(2) Maombi ya idhini chini ya kanuni ndogo ya (1) yataainisha-

(a) wahusika anaokutana nao;
(b) suala litakalojadiliwa; na
(c) muda na sehemu wanayokutana.

(3) Maombi ya idhini chini ya kanuni ndogo ya (1) yatafanywa na mwanafunzi kwa maandishi na endapo yatafanywa na kikundi cha wanafunzi, yatapitia kwa mwakilishi wa wanafunzi.

Ruhusa

**7**.-(1) Mwanafunzi anayetaka kusafiri nje ya Mkoa wakati wa kipindi cha mafunzo ataomba ruhusa ya kimaandishi kwa-

(a) ikiwa ni safari ya siku zisizozidi tano, Mshauri wa Wanafunzi;
(b) ikiwa ni safari ya siku zinazozidi tano, Naibu Mkuu wa Shule Mafunzo, Tafiti na Machapisho; na
(c) ikiwa ni safari wakati wa mapumziko ya mwisho wa wiki au sikukuu, Mshauri wa Wanafunzi.

(2) Mwanafunzi anayesafiri nje ya nchi wakati wa kipindi cha mafunzo ataomba ruhusa ya kimaandishi kwa Mkuu wa Shule.

Kukusanya fedha

**8**.-(1) Mwanafunzi hataruhusiwa kukusanya fedha au kufanya harambee kwa kutumia jina la Shule bila idhini ya Shule.

(2) Maombi ya idhini ya kukusanya fedha au harambee yatafanywa kwa Mshauri wa Wanafunzi kwa maandishi kupitia Jumuiya ya Wanafunzi na maombi hayo yataambatishwa na maelezo yenye sababu ya kukusanya fedha au harambee hiyo.

(3) Mwanafunzi anayekusanya fedha au kufanya harambee atahakikisha kuwa fedha zilizokusanywa zinawekwa katika akaunti ya Jumuiya ya Wanafunzi na ushahidi wa makusanyo hayo ukionyesha matumizi ya fedha hizo utawasilishwa kwa Mshauri wa Wanafunzi.

## SEHEMU YA TATU
## MASUALA YA NIDHAMU

Kulinda taswira ya Shule

**9**. Mwanafunzi hatakuwa na mwenendo ambao unachafua taswira ya Shule.

Mamlaka ya nidhamu

**10**. Mamlaka ya kusimamia nidhamu ya wanafunzi katika Shule yatakuwa ni-

(a) Mshauri wa Wanafunzi;

(b) Kamati ya Ustawi na Nidhamu ya Wanafunzi; na

(c) Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wanafunzi.

Mshauri wa Wanafunzi

**11**.-(1) Mshauri wa Wanafunzi atakuwa na mamlaka ya kutoa onyo, karipio au kumtaka mwanafunzi aliyekiuka Kanuni hizi kurekebisha makosa yake.

(2) Mwanafunzi ambaye hajaridhika na onyo, karipio au maelekezo mengine yoyote yaliyotolewa na Mshauri wa Wanafunzi chini ya kanuni ndogo ya (1) anaweza kumuomba Mshauri wa Wanafunzi kwa maandishi kuwasilisha suala lake kwenye Kamati ya Ustawi na Nidhamu ya Wanafunzi ndani ya siku tano za kazi.

(3) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (2), Mshauri wa Wanafunzi atawasilisha maombi hayo kwa Kamati ya Ustawi na Nidhamu ya Wanafunzi ndani ya siku saba baada ya kupokea maombi hayo.

Kamati ya Ustawi na Nidhamu ya Wanafunzi

**12**.-(1) Kamati ya Ustawi na Nidhamu ya Wanafunzi itaundwa na Mkuu wa Shule na itajumuisha wajumbe wafuatao:

(a) afisa mwandamizi kutoka ofisi yoyote ndani ya Shule ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) mjumbe mmoja kutoka Idara ya Sheria ambaye atakuwa Katibu;

(c) afisa mwandamizi kutoka Idara ya Maktaba;

(d) mjumbe mmoja kutoka Kurugenzi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo; na

(e) mwakilishi mmoja wa wanafunzi aliyeteuliwa na rais wa Jumuiya ya Wanafunzi.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Ustawi na Nidhamu ya Wanafunzi watahudumu kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja cha miaka mitatu.

(3) Akidi ya Kamati ya Ustawi na Nidhamu ya Wanafunzi itakuwa ni wajumbe wa tatu waliohudhuria kikao.

(4) Kamati ya Ustawi na Nidhamu ya Wanafunzi itakuwa na mamlaka ya kutoa adhabu kwa wanafunzi waliotenda makosa ya kinidhamu yaliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wanafunzi

**13**.-(1) Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wanafunzi itaundwa na Mkuu wa Shule na itajumuisha wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti;

(b) Katibu; na

(c) wajumbe wengine watatu ambapo mjumbe mmojawapo atakuwa ni mwakilishi wa wanafunzi.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wanafunzi watahudumu kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja cha miaka mitatu.

(3) Akidi ya Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wanafunzi itakuwa ni wajumbe watatu waliohudhuria kikao.

(4) Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wanafunzi itakuwa na mamlaka ya kusikiliza rufaa kwa wanafunzi ambao hawajaridhika na maamuzi ya Kamati ya Ustawi na Nidhamu ya Wanafunzi.

Malalamiko

**14**.-(1) Malalamiko yote yanayohusiana na ukiukwaji wa Kanuni hizi yatawasilishwa kwa maandishi kwa Mshauri wa Wanafunzi.

(2) Mshauri wa Wanafunzi baada ya kupokea malalamiko atafanya uchunguzi wa malalamiko hayo na

kuchukua hatua stahiki.

(3) Endapo mwanafunzi ana lalamiko dhidi ya mtumishi wa Shule Mshauri wa Wanafunzi atawasilisha lalamiko kwa Mkuu wa Kitengo au Kurugenzi inayohusika na mtumishi huyo.

(4) Endapo Mkuu wa Kitengo au Kurugenzi aliyerejewa chini ya kanuni ndogo ya (3) atashindwa kutatua malalamiko yaliyowasilishwa kwake, atawasilisha malalamiko hayo kwa mamlaka za juu za kinidhamu za mtumishi huyo.

Rufaa

**15**.-(1) Mtu ambaye hajaridhika na Uamuzi wa Kamati ya Ustawi na Nidhamu ya Wanafunzi anaweza kukata rufaa kwa Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wanafunzi ndani ya siku saba kutoka tarehe ya uamuzi.

(2) Rufaa chini ya kanuni ndogo ya (1) itawasilishwa kwa maandishi na kuainisha sababu za rufaa.

(3) Rufaa iliyowasilishwa chini ya kanuni ndogo ya (1), itasimamisha papo hapo adhabu iliyotolewa na Kamati ya Ustawi na Nidhamu ya Wanafunzi kusubiria uamuzi wa rufaa.

(4) Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wanafunzi inaweza kuongeza muda wa kukata rufaa baada ya kupokea maombi ya maandishi ya kuongeza muda wa kukata rufaa.

(5) Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wanafunzi baada ya kupokea rufaa itakutana ndani ya siku saba za kazi na kuamua rufaa hiyo.

(6) Mjumbe wa Kamati ya Ustawi na Nidhamu ya Wanafunzi ambaye alishiriki katika kutoa uamuzi katika shauri linalokatiwa rufaa hataruhusiwa kusikiliza rufaa.

(7) Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wanafunzi wakati wa kusikiliza rufaa itakuwa na mamlaka ya kuthibitisha au kufuta uamuzi wa Kamati ya Ustawi na Nidhamu ya Wanafunzi na itatoa sababu ya kufanya uamuzi huo.

(8) Uamuzi wa Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wanafunzi utakuwa wa mwisho.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA JUMLA

Mali za wanafunzi

**16**. Shule haitakuwa na jukumu la kutunza na kulinda mali za wanafunzi.

Malazi na chakula

**17**. Mwanafunzi atakuwa na jukumu la kujigharamia malazi na chakula.

Mahitaji maalumu

**18**. Mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu atawasilisha cheti cha daktari kinachothibitisha mahitaji kwa Mkuu wa Shule kwa ajili ya kupata msaada unaohitajika.

Mavazi

**19**. Mwanafunzi atazingatia waraka wa mavazi kama ulivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Huduma za maktaba

**20**. Mwanafunzi au mtahiniwa atazingatia kanuni za maktaba.

Gharama za kusimamishwa masomo

**21**. Mwanafunzi ambaye atarejea masomoni baada ya kusimamishwa kwa kosa lolote aliloadhibiwa kwa mujibu wa Kanuni hizi atagharamia gharama zote zinazohitajika.

Mazishi

**22**. Endapo mwanafunzi atafariki, Shule itashiriki kwenye taratibu za mazishi na kugharamia msiba kama itakavyoona inafaa.

Makosa ya jinai

**23**.-(1) Mwanafunzi atakayetiwa hatiani kwa kosa la jinai atakoma kuwa mwanafunzi wa Shule.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), endapo mwanafunzi aliyetiwa hatiani kwa kosa la jinai atashinda dhidi ya uamuzi huo kupitia rufaa atarudishwa Shule na kuendelea na masomo pale alipoishia.

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA · THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA · PROFESSIONALISM & EXCELLENCE

*Tangazo la Serikali Na.619 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 12(4))*

MAKOSA NA ADHABU

| NA. | MAKOSA | KUTENDA KOSA KWA MARA YA KWANZA | KUTENDA KOSA KWA MARA YA PILI | KUTENDA KOSA KWA MARA YA TATU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kupiga kelele au kufanya usumbufu au kukusanya wanafunzi wengine au watu kwa ajili ya kupiga kelele au kufanya usumbufu wa aina yoyote katika eneo la Shule. | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kufukuzwa Shule |
| 2. | Kupanga au kushiriki kwenye migomo ya masomo. | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kusimamishwa masomo kwa siku 90 | Kufukuzwa Shule |
| 3. | Kupanga au kushiriki au kushawishi wengine kushiriki kwenye mikusanyiko isiyo ya halali. | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kusimamishwa masomo kwa siku 90 | Kufukuzwa Shule |
| 4. | Kulewa au kunywa pombe katika eneo la shule | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kufukuzwa Shule |
| 5. | Kufanya matendo yoyote yanayopelekea uharibifu wa mali za Shule au za wanafunzi au za watu waliopo katika eneo la Shule. | Onyo kali | Fidia inayolingana na uharibifu uliofanyika | Kulipa fidia ya uharibifu alioufanya na kufukuzwa Shule |
| 6. | Kufanya au kupanga au kushawishi wanafunzi wengine kushiriki kufanya vurugu kwa wanafunzi wenzao au watu waliopo katika eneo la Shule. | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kufukuzwa Shule |
| 7. | Kutoa lugha ya matusi, kushutumu au kumkera mwanafunzi mwenzake, mtumishi wa Shule au familia zao. | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kufukuzwa Shule |
| 8. | Kutupa takataka au kufanya uchafuzi wa mazingira katika eneo la Shule. | Onyo | Onyo kali | Faini isiyozidi shilingi laki moja |
| 9. | Kuvuta sigara katika eneo la Shule. | Onyo | Onyo kali | Faini isiyozidi shilingi laki moja |

*Tangazo la Serikali Na.619 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10. | Kufanya kitendo chochote cha kuzuia, kupinga au kitendo kinachoweza kuzuia au kupinga utekelezaji wa shughuli halali zilizopangwa kufanyika Shule. | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kufukuzwa Shule |
| 11. | Kutoa taarifa za uongo, kushindwa kujitambulisha au kutoa kitambulisho pindi atakapohitajika kufanya hivyo na Afisa wa Shule mwenye mamlaka ya kudai taarifa au kitambulisho ili kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria. | Onyo | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 |
| 12. | Kufanya uharibifu wa makusudi kwa kudhamiria au kwa uzembe na kuteketeza Miti, Uzio wa Michongoma, Maua, Uzio au kitu chochote kilichopo ndani ya maeneo ya Shule na ambacho kipo chini ya uangalizi wa Shule. | Onyo kali | Faini isiyozidi shilingi laki moja | Kusimamishwa masomo kwa siku 60 |
| 13. | Kumkaribisha, kumkarimu, kumficha mhalifu au mtu yeyote ambaye amezuiliwa kuingia kwenye maeneo ya Shule. | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kufukuzwa Shule |
| 14. | Kuacha kufanya au kukataa kutekeleza amri halali iliyotolewa na Shule au kukataa kutekeleza uamuzi au maelekezo yaliyotolewa na chombo cha Shule chenye mamlaka. | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kusimamishwa masomo kwa siku 90 | Kufukuzwa Shule |
| 15. | Kumiliki rasilimali ya Shule kwa njia isiyokuwa ya halali. | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kufukuzwa Shule |
| 16. | Kuzuia kwa makusudi au kupinga au kusababisha kuzuia kufanyika kwa kazi au utaratibu halali uliowekwa na Shule, mwenendo wa muhimili wa Shule uliyoundwa kwa mujibu wa sheria. | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kusimamishwa masomo kwa siku 60 |
| 17. | Kutumia rasilimali za Shule kwa matumizi binafsi bila ya kuwa na kibali kutoka kwa afisa mfawidhi wa kitengo au kurugenzi husika na kutoa huduma hiyo. | Onyo | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 |

*Tangazo la Serikali Na.619 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 18. | Kumshambulia mwanafunzi mwenzake au mdau yeyote wa Shule. | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kufukuzwa Shule |
| 19. | Kumtishia Maisha mwanafunzi mwenzake au mdau wa Shule au kumsababishia majeraha ya kimwili kwa sababu zozote. | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kusimamishwa masomo kwa siku 90 | Kufukuzwa Shule |
| 20. | Kutumia ujuzi wa Tehama na vifaa vya kiteknolojia kwa namna isiyokubalika au kutumia ujuzi wa Tehama kwenye kuvunja sheria na kanuni za Shule. | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kusimamishwa masomo kwa siku 60 |
| 21. | Kubandika matangazo, mabango, alama au vitu vyovyote vya aina hiyo kwenye maeneo ya Shule bila kibali. | Onyo | Onyo kali | Kusimamishwa masomo siku 30 |
| 22. | Mwanafunzi kutengeneza mazingira ya kutishia, ushindani, chuki, kushambulia au kutoa elimu ya masuala yaliyokatazwa kisheria au kinyume na utaratibu wa Shule. | Onyo | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 |
| 23. | Kuingilia njia ya mawasiliano, mfumo au mawimbi ya hewa kwa sababu yeyote ile ili kuweza kupata taarifa ya ujumbe uliofichwa kwa wanafunzi wengine na wadau wa Shule kwa dhumuni la kufanya kitu kilicho kinyume na sheria. | Kufukuzwa Shule | | |
| 24. | Kufanya utani au kutoa viashiria, mapendekezo ya kingono, ishara chafu kwa mwanafunzi, mkufunzi au watumishi wa Shule. | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kusimamishwa masomo kwa siku 60 |
| 25. | Kutoa maneno ya dharau kwa mtu. | Onyo | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 |
| 26. | Kushinikiza matendo ya kingono au upendeleo. | Onyo | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 |
| 27. | Kuongea uongo au kusambaza tetesi kuhusiana na maisha ya mtu ya kimahusiano kwa lengo la kumchafulia taswira mhusika au muhanga. | Onyo | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 |
| 28. | Kuwa na migusano ya | Onyo kali | Kusimamishwa | Kufukuzwa |

*Tangazo la Serikali Na.619 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | kimwili isiyotakiwa ambayo ina viashiria vya kingono inayohusisha kugusa sehemu nyeti za mwili, kusugua, kubusu, kufinya, kukamata au kupapasa mwili, nywele, nguo za mtu mwingine. | | masomo kwa siku 30 | Shule |
| 29. | Kuonyesha picha za ngono au picha zenye ushawishi wa kingono. | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kufukuzwa Shule |
| 30. | Kusambaza masuala yenye viashiria vya kingono kwa njia ya maandishi, simu au mtandao. | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kusimamishwa masomo kwa siku 90 | Kufukuzwa Shule |
| 31. | Kutumia nguvu, kwa uwazi au kwa kificho kumlazimisha mwingine kuingia kwenye mahusiano ya kingono. | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kufukuzwa Shule |
| 32. | Kusaidia kuwezesha vitendo vya unyanyasaji wa kingono. | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kusimamishwa masomo kwa siku 60 | Kufukuzwa Shule |
| 33. | Kuchapisha au kusababisha kuchapishwa kwa njia ya kimtandao au ujuzi wa Tehama picha za Ngono au picha za uzinifu. | Kusimamishwa masomo kwa siku 60 | Kufukuzwa Shule | |
| 34. | Kuchapisha taarifa za kingono kwa njia ya picha, maandishi, alama au njia yoyote inayopitishwa kwenye mifumo ya Tehama huku akijua taarifa hiyo ni ya uongo, inapotosha, sio sahihi, inatishia, na kuchafua taswira ya Shule na umma kwa ujumla. | Kusimamishwa masomo kwa siku 60 | Kufukuzwa Shule | |
| 35. | Kuanzisha au kutuma mawasiliano ya kingono kwa njia ya mtandao kwa mtu mwingine kwa lengo la kumlazimisha, kumtishia, kumnyanyasa au kusababisha maumivu ya kihisia. | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 60 | Kufukuzwa Shule |
| 36. | Kuanzisha au kusaidia kurusha taarifa zenye maudhui ya za kingono | Onyo kali | Kusimamishwa masomo kwa siku 30 | Kufukuzwa Shule |

JEDWALI LA PILI

*(Limetemgenezwa chini ya kanuni ya 19)*

KANUNI ZA MAVAZI KWA WANAFUNZI

Kanuni hizi za Mavazi zimezingatia Waraka wa Mavazi kwa watumishi wa umma kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Maadili za Mawakili.

Hivyo basi mavazi ya wanafunzi yatakuwa kama ifuatavyo:

1. Siku ya jumatatu mwanafunzi wa kiume anatakiwa kuvaa vazi rasmi la suti nyeusi, bluu iliyokoza au kijivu na shati jeupe au bluu bahari na mwanafunzi wa kike watavaa blauzi nyeupe au ya bluu bahari na viatu vyeusi au rangi ya ugoro. Mwanafunzi wa kike anaweza kuvaa suti za sketi au suruali.

2. Katika kipindi cha mafunzo ya vitendo, mahakama za mafunzo na mazoezi mengine ya aina hiyo kama itakavyoshauriwa na mratibu wa kozi, mwanafunzi anatakiwa kuvaa vazi rasmi.

3. Siku nyingine za kawaida mwanafunzi anatakiwa avae mavazi ya kawaida kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika Chati hapa chini-

| Na. | Mavazi yasiyoruhusiwa kwa mwanafunzi wa kike | Mavazi yasiyoruhusiwa kwa mwanafunzi wa kiume | Masharti ya jumla ya mavazi yasiyoruhusiwa kwa wanafunzi wote wa kike na wa kiume |
|---|---|---|---|
| 1. | Suruali, Sketi au Magauni ya kubana na kuonyesha maungo ya mwili. | Suruali zilizochoka. | Mavazi yanayoonyesha maeneo ya mgongo, kifua, miguu, tumbo na nguo za ndani hayatakiwi kuvaliwa ndani ya maeneo ya Shule. |
| 2. | Suruali ya Kubana. | Mashati yasiyokuwa na vishikizo au mashati yasiyokuwa na mikono. | Suruali na sketi zisizotosha kiunoni na zisizopindwa vizuri na kuishia chini ya magoti ambazo haziburuzi chini. “Mlegezo/ “Kata K” |
| 3. | Magauni au sketi fupi ambazo zipo juu ya magoti. Mavazi yote yanatakiwa kuwa na urefu mpaka magotini au chini ya magoti. | Mavazi yanayoonyesha kiwiliwili. | Mavazi yote rasmi na yasiyo rasmi yanatakiwa yawe masafi, yaliyonyooshwa, yasiwe na mikunjo wala matundu na madoadoa. |
| 4. | Mavazi yenye mpasuo juu ya magoti. | Vitambaa vya kuvaa kichwani. | Nguo zenye maneno, vigezo au picha ambazo zinashambulia watu wengine. Mavazi yenye |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | ujumbe wa kisiasa. |
| 5. | Mavazi yanayoonyesha viungo vya mwili kama; tumbo, matiti, kiuno au mapaja. | Mwanafunzi wa kiume hatakiwi kusuka nywele, kufuga rasta, kuvaa hereni au kufuga ndevu za mapambo. | Kaptura, bukta, suruali za *jeans*. |
| 6. | Nguo za kuonyesha maungo ya mwili. | Ndevu zinatakiwa zinyolewe na kutunzwa vizuri. | Migongo wazi, tisheti za mabega wazi, tisheti zinazoacha matumbo wazi. |
| 7. | | | Miwani ya jua haitakiwi kuvaliwa ndani ya majengo kwenye maeneo ya Shule. |

*Mwanafunzi ambaye atakiuka kanuni za mavazi atatakiwa kurudi nyumbani kubadilisha mavazi aliyovaa.

Dar es Salaam, KENNEDY G. GASTORN,
8 Julai, 2024 *Mwenyekiti wa Bodi*

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA